




# YUKO WAPI RAFIKI YANGU?

Mtunzi: Tebogo Maganye

Mchoraji: Michael Sagikwa






Nia hamuoni rafiki yake.  
Kila wakati huwa anajificha.  
Nia anapata taabu kumtafuta.  
Nia anawaza...  
Oh! Nia amepata suluhisho.



Siku ya Jumatatu,  
alimpaka rangi  
nyekundu. Ili  
amuone kwa urahisi  
“Uko wapi?” Nia  
anamtafuta.






“Niko kwenye matufaa mekundu.”



Siku ya Jumanne alimpaka rangi  
ya chungwa ili amuone kwa urahisi.





Rafiki yake akajificha kwenye matunda.



Siku ya Jumatano nayo alipaka  
rangi ya manjano. Nikimpaka  
rangi hii nitamuona kwa urahisi.





Tazama niko huku.





Siku ya Alhamisi, aliamua kupaka  
rangi ya kijani.






Tazama rafiki yake Nia alikojificha.





Siku ya Ijumaa, alipaka rangi  
ya samawati.



Rafiki alijificha kwenye picha  
iliyobandikwa ukutani.



Siku ya Jumamosi alipaka yangi  
ya zambarau.





Alijificha kwenye zabibu mbivu.



Siku ya Jumapili, Nia alipata suluhisho. Alipaka rangi za upinde wa mvua.



Oh! Leo rafiki yake nia hana  
tena pa kujificha. Anaonekana  
kwa urahisi.